

Je, Canopy hufanya nini?

Sisi hurekebisha nyumba mahame katika Leeds ili kuboresha mazingira ya hapa.

Tunatoa nafasi kwa watu wajitolee ili kusaidia kupaka rangi na kupamba nyumba mahame, kujifunza ujuzi, kupatana na watu na kuwa sehemu ya timu.

Tunaunda nyumba zilizorekebisha zenye kumudika kwa familia na watu waliyo kivyao ambao hawana mahali pa kuishi au wako katika hatari ya kutokuwa na makao.

Canopy iko mahali panapokaribisha ambapo unaweza kujua kutumia mchana, iliyo na jikoni, kompyuta, simu, na mpira wa miguu wa mezani.

Canopy hufanya kazi kiviipi?

Kwanza kabisa Canopy hutafuta nyumba zilizo wazi, zilizo na milango ya mabati na zinazokera watu katika mtaa huo. Kisha tunafanya mipango kwa usaidizi wa kabaila ya kuchukua nyumba hiyo na tunapanga mafundi wa stima, mafundi wa bomba na wa paa wakamilishe kazi zote kubwa.

Kisha wafanyikazi wa Canopy, wanaojitolea na wapangaji huingia nyumba hiyo na vifaa na kuweka plasta, vigae, karatasi za ukutani na rangi. Mtu au familia ambayo inaishi katika nyumba hii, itafanya kazi kama sehemu ya timu ya wanaojitolea ili kurekebisha nyumba watakaohamia na watachagua rangi watakayopaka nyumba yao.

Tayari tumefanya kazi katika maeneo mawili katika Leeds tangu 1998 (Hyde Park na Beeston), na tutaanza mradi hivi karibuni katika Harehills.

Je, ni nani wanaojitolea kwa Canopy?

Watu wa mtaani, vijana, watu wazee, wanaume na wanawake na watu wa mataifa tofauti hujitolea kwa Canopy. Sisi wote hujifunza mambo tofauti kutoka kwetu wenyewe pamoja na jinsi ya kupamba na kufanya kazi ya ujenzi, jinsi ya kuzungumza lugha tofauti. Tuna timu ya mpira wa miguu, tuna siku za kujivinjari, kucheza mpira wa miguu wa mezani na zaidi. Tunaangalia filamu na baadhi ya picha zetu kwa <http://www.canopyhousingproject.org/gallery.html>

Je, ni kwanini watu hujitolea?

Wengi wa watu wetu wanaojitolea huenda kwa kozi za mafunzo au mwishowe hupata kazi, wengine hufurahia maarifa ya kuwa sehemu ya timu nzuri ambayo kila mtu anakaribishwa na anaweza kusaidia watu wengine na kufanya nyumba za hapa kuonekana mpya tena. Canopy inaweza kutafuta mkalimani ikiwa unahitaji mmoja. Kufanya kazi katika eneo na wengine wanaojitolea ni fursa kubwa ya kujifunza na kuzoea Kiingereza nje ya darasa.

Je, unaweza kuhusika?

Unaweza kupenda kujitolea kusaidia kurekebisha nyumba mahame au unaweza kuwa unawajua watu wengine ambao wanaweza kupenda kujitolea. Unaweza kujifunza ujuzi, kupata msaada wa kutafuta kazi, au kukutana na watu wengine, tupigie simu 2946868.

Je, unahitaji nyumba? Ikiwa hauna makao na uko tayari kupamba nyumba yako mpya kwa usaidizi kutoka kwa timu ya wanaojitolea, basi piga simu Canopy ili ujue kama kuna nyumba zozote zinazopatikana.

**Ikiwa ungependa kujitolea au kuwa mpangaji tafadhali piga simu Canopy
0113 2946868**